

Inakisiwa kwamba lugha ya Kiswahili huzungumzwa na zaidi ya watu milioni 100 ulimwenguni kote. Kati ya wazungumzaji hawa, ni takriban watu milioni mbili tu ambao wanazungumza Kiswahili kama lugha ya mama. Vilevile, mbali na Kiarabu, Kiswahili ndiyo lugha ya Kiafrika yenye wazungumzaji wengi zaidi ulimwenguni. Hali hii inamaanisha kwamba Kiswahili kinaendelea kutanda na kuenea katika pembe zote za ulimwengu na kufika katika janibu za mbali kutoka katika chimbuko lake. Hivi sasa, Kiswahili kinafundishwa na kutafitiwa katika vyuo vikuu mbalimbali sio tu hapa barani Afrika, bali pia Marekeni, Ulaya, Asia na kwa hakika ulimwenguni kote. Isitoshe, Kiswahili ni lugha ya mawasiliano katika Afrika Mashariki na Kati pamoja na kwamba ni lugha taifa na/au lugha rasmi katika mataifa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kukua, kusambaa na kuimarike kwa Kiswahili kumetokana na sababu mbalimbali kama vile biashara, ushirikiano wa kimataifa, utalii na usafiri na utandawazi miongoni mwa sababu zingine. Pamoja na hayo, kuna asasi nyingi ambazo huhusika katika ukuzaji na uendelezaji wa Kiswahili katika mataifa na maeneo tofautitofauti. Asasi hizo ni pamoja na taasisi za elimu, bunge na vyombo nya utungaji sera, vyombo nya habari na mawasiliano, idara za Kiswahili katika vyuo vikuu, dini, sekta ya uchapishaji, na kadhalika. Katika *UkuzaJI wa Kiswahili: Dhima na Majukumu ya Asasi Mbalimbali*, wataalamu watajika wa Kiswahili wanachanganua na kutathmini mchango wa asasi hizo katika ukuzaji wa Kiswahili. Wataalamu hao wametoka mataifa tofautitofauti kama vile Unguja, Marekani, Urusi, Japani, Tanzania na Kenya. Aidha, wataalamu hao wanaangazia changamoto zilizoko na kutoa mapendekezo ambayo yakizingatiwa, yatapelekea Kiswahili kuimarike hata zaidi ili kiweze kuwa chombo mufti cha mawasiliano, ustawi na maendeleo katika nyakati hizi za utandawazi na teknojia ya habari na mawasiliano. Hiki ni kitabu muhimu kwa wapenzi na wasomi wa Kiswahili.

ISBN: 9966-01-211-9



9 879966 012119



UKUZAJI WA KISWAHILI

UKUZAJI WA KISWAHILI

Dhima na Majukumu ya Asasi Mbalimbali



Nyachae Michira • P.I. Iribemwangi
Mwenda Mbatiah

Nyachae Michira • P.I. Iribemwangi • Mwenda Mbatiah
(Wahariri)

